# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

## UGAWAJI WA VITAMBULISHO VYA WAFANYABIASHARA WADOGO NA WATOA HUDUMA KWA MWAKA 2021 NA MIAKA IJAYO

## 11 FEBRUARI 2021

# YALIYOMO


1.0 UTANGULIZI

2.0 TAFSIRI YA MFANYABIASHARA MDOGO NA MTOA HUDUMA MDOGO

3.0 SHERIA HUSIKA KWA WAFANYABIASHARA WADOGO NA WATOA HUDUMA WADOGO

4.0 UTARATIBU WA UOMBAJI WA VITAMBULISHO

5.0 MUOMBAJI MWENYE KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIN) AU LESENI YA UDEREVA

6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

7.0 MFUMO WA NDANI WA KUFANYIA KAZI MAOMBI YA USAJILI

8.0 HITIMISHO

# 1.0 UTANGULIZI

- Zoezi la ugawaji wa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo maarufu kwa jina la Machinga lilianzishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Dr. John Pombe Joseph Magufuli** tarehe 10 Desemba 2018.
- Lengo likiwa, ni kuliandaa na kulikuza kundi hili la wafanyabiashara linalojishughulisha na kazi za kiuchumi ili siku za usoni, baada ya kukua kwa biashara zao, liingizwe kwenye wigo rasmi wa kodi kwa mujibu wa Sheria

# UTANGULIZI unaendelea…

- **Majukumu ya usimamizi**

- Majukumu ya usimamizi wa vitambulisho yamegawanywa katika mafungu mawili;
    - Jukumu la kuwatambua, kuhamasisha na kugawa vitambulisho kwa waombaji litakuwa chini ya Serikali za Mitaa.
    - TRA itakuwa na jukumu la kuchapisha na kuhasibu mapato yatokanayo na Ada za vitambulisho.

# UTANGULIZI unaendelea…

## ❑ Upokeaji, Uchapishaji na Usambazaji

- Maombi ya kitambulisho yatapokelewa katika Mkoa wa Kodi husika kupitia mfumo wa kielektroniki;
- Meneja wa Mkoa wa Kodi atahitajika kuchapisha na kuandaa vitambulisho baada ya kupokea maombi hayo;
- Baada ya uandaaji wa vitambulisho, Meneja wa Mkoa husika atawajibika kuvisambaza katika Halmashauri husika ili viweze kuwasilishwa kwa Waombaji;

# UTANGULIZI unaendelea…

- Vilevile, Meneja wa Mkoa wa Kodi husika atatakiwa kuandaa taarifa kila mwezi ya vitambulisho vilivyotolewa na kuwasilisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa husika;
- Muombaji atatakiwa kuchukua kitambulisho katika Ofisi ya Halmashauri husika.

# 2.0 TAFSIRI YA MFANYABIASHARA MDOGO NA MTOA HUDUMA MDOGO

- Kwa mujibu wa **Sheria ya Kodi ya Mapato,Sura ya 332,** kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria hiyo ni yule ambaye mauzo ghafi ya bidhaa, huduma au vyote kwa pamoja, hayazidi kiasi cha **Fedha za Kitanzania Shilingi Milioni Nne Tu (TZS 4,000,000/=) kwa mwaka**
- Awe hajasajiliwa kama mfanyabiashara na kupewa **TIN ya biashara** na TRA
- **Mauzo ghafi,** ni jumla ya mauzo yote yanayofanyika bila kutoa gharama za uzalishaji wa bidhaa au huduma (au vyote kwa pamoja) zinazotolewa.
- Mauzo ghafi ni tofauti na **mtaji** au **faida** anayoipata mfanyabiashara.

# 3.0 SHERIA HUSIKA KWA WAFANYABIASHARA WADOGO NA WATOA HUDUMA WADOGO

- Kifungu cha **22A (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015, Sura ya 438 (R.E 2017)** kinamtaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo waliopo katika sekta isiyo rasmi.
- Aidha, Kifungu cha **22(A)** cha Sheria tajwa, pia kinamtaka Kamishna Mkuu TRA, kuwapatia kadi za utambulisho wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo waliosajiliwa.

# 3.0 SHERIA HUSIKA KWA WAFANYABIASHARA WADOGO NA WATOA HUDUMA WADOGO ….Inaendelea

- Aidha, Kanuni ya 6 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi (Usajili wa Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma wadogo) za Mwaka 2020 inamtaka Kamishna Mkuu (TRA) kumpatia Mfanyabiashara mdogo na Mtoa Huduma Mdogo kitambulisho baada ya kukamilisha malipo ya ada ya **Shilingi za Kitanzania Elfu Ishirini tu (TZS 20,000/=)**

# 4.0 UTARATIBU WA UOMBAJI WA VITAMBULISHO

- Maombi ya kitambulisho yatafanyika kupitia mfumo wa kielektroniki unaopatikana kupitia:-
- Kupitia tovuti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa (TAMISEMI) wwww.tamisemi.go.tz;
- Programu tumizi ya mfumo wa machinga (Machinga App) ambayo inapatikana "play store".
- Mfumo huo utakuwa na uwezo wa kutoa **namba ya kumbukumbu ya maombi** na **namba ya malipo** baada ya taarifa za Muombaji kukamilika.

# 4.0 UTARATIBU WA UOMBAJI … Inaendelea

- Maombi ya kitambulisho yanaweza kufanyika kwa njia zifuatazo;
  - Muombaji ambaye ana kitambulisho cha Taifa au leseni ya Udereva ataweza kujisajili mwenyewe kupitia mtandao www.tamisemi.go.tz au simu janja ya mkononi na kufanya usajili mwenyewe;
  - Muombaji ambaye hana kitambulisho cha Taifa au leseni ya udereva ataweza kujisajili kupitia simu janja ya mkononi kwa kupakua Machinga App. na kujisajili mwenyewe na;
  - Kwa wale ambao watashindwa kutumia njia hizo hapo juu, watatakiwa kwenda katika Ofisi za Halmashauri zilizo jirani yao ili waweze kupata msaada wa kujisajili.

# 5.0 MUOMBAJI MWENYE KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIN) AU LESENI YA UDEREVA

1. Muombaji ataingia katika tovuti ya Tamisemi www.tamisemi.go.tz na kufungua sehemu ya Usajili wa Wamachinga, baada ya ukurasa huo kufunguka atabofya kitufe cha “***Omba Kitambulisho kipya***”



# 5.0 MUOMBAJI MWENYE KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIN) AU LESENI YA UDEREVA………

2. Muombaji atatakiwa kuingiza namba ya kitambulisho cha Taifa **(NIN) au namba ya Leseni ya Udereva**



# 5.0 MUOMBAJI MWENYE KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIN) AU LESENI YA UDEREVA………

3. Taarifa binafsi za Muombaji zitatokea na Muombaji atatakiwa kujaza taarifa zake kwa usahihi na kisha kubofya “***Wasilisha Maombi***”



## 5.0 MUOMBAJI MWENYE KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIN) AU LESENI YA UDEREVA………

- Baada ya kuwasilisha maombi, Muombaji atatumiwa namba ya kumbukumbu ambayo atatakiwa kuitunza kwani atatakiwa kutaitumia ili kupata taarifa za maombi na malipo yake.
- Vilevile, baada ya kuwasilisha maombi atatumiwa ujumbe mfupi kwenye simu yake, utakaonyesha bili pamoja na namba ya malipo kwa ajili ya kufanya malipo kupitia mfumo wa malipo wa serikali.

# 5.0 MUOMBAJI MWENYE KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIN) AU LESENI YA UDEREVA………

4. Kujua taarifa za maombi au malipo , Muombaji atatakiwa kubofya "***Taarifa ya maombi yako***" au "***Taarifa ya malipo yako***".



# 5.0 MUOMBAJI MWENYE KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIN) AU LESENI YA UDEREVA………

5. Muombaji atatakiwa kuweka namba ya kumbukumbu aliyotumiwa awali na kubofya “***Tafuta***”



# 5.0 MUOMBAJI MWENYE KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIN) AU LESENI YA UDEREVA………

6. Muombaji atapata taarifa zake kama inavyoonekana hapa chini:



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

- **Maombi kwa kupitia tovuti**,

1. Muombaji ataingia na kuchagua usajili wa Wamachinga na kubofya "***Omba Kitambulisho Kipya***" kisha ***"Sina Kitambulisho"***.



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO …

2. Muombaji atajaza taarifa zake kwa usahihi kwenye fomu, kisha ataweka picha yake kwa kubofya “***browse***” ikifuatiwa na “***wasilisha maombi***”.



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

- **Maombi kwa kupitia Simu janja ya Mkononi (Mobile APP)**,
- Njia hii ya maombi, Muombaji atatakia kuwa na simu ya mkononi yenye mfumo wa aina ya “**Android**”.
- Atatakiwa kwenda kwenye sehemu ya kuhifadhi mifumo mbalimbali ya simu “Appstore” na kupakua mfumo wa “Application ya “machinga” na kiiweka kwenye simu yake.

# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

1. Muombaji atafungua **Application ya Machinga** iliyopo kwenye simu yake, na kubofya “***Omba Kitambulisho”;***



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

2. Muombaji atatakiwa kuweka namba yake ya simu, na kubofya “***Endelea”;***



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

**3.** Muombaji atatakiwa kubofya "***Sina Kitambulisho***" na kisha "***Endelea";***



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

**3.** Muombaji atatakiwa kubofya “***Piga Picha”*** au ***“Chagua Iliyopo”;***



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

**4.** Muombaji atatakiwa kuchagua “**Mkoa**”, ”**Wilaya** ” na “**eneo la biashara**” kisha bofya “**endelea**”



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

**5.** Muombaji atatakiwa kujaza taarifa zake kwa sahihi na kubofya “**endelea**” baada ya kukamilisha ujazaji;



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

**6.** Muombaji atatakiwa kuchagua “aina ya biashara”, “**muda wa makadirio**” na“**mauzo**” kisha bofya “**endelea”;**



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

**7.** Muombaji atapokea namba ya kumbukumu ya maombi na kutakiwa kuihifadhi sehemu salama;



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

**8.** Kuweza kuangalia taarifa za maombi**,** Muombaji atabofya “ ***Kumbukumbu Namba”*** ;



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

9. Muombaji ataweka Namba ya kumbukumbu ya maombi kisha kubofya “***Angalia***”



# 6.0 MUOMBAJI AMBAYE HANA KITAMBULISHO

10. Taarifa za Muombaji zitajitokeza kama inavyoonekana hapa chini;



# 7.0 MFUMO WA NDANI WA KUFANYIA KAZI MAOMBI YA USAJILI

- Afisa wa TAMISEMI/TRA atabofya hapa http://192.168.80.89:8000 na mfumo wa ndani utafunguka;
- Ili kuweza kuingia kwenye mfumo mtumiaji atatakiwa kuwa amesajiliwa na kupatiwa "***jina tambulishi***" na "***neno siri***"

# 7.0 MFUMO WA NDANI WA KUFANYIA KAZI MAOMBI YA USAJILI…

1. Kuingia kwenye mfumo, mtumiaji atatakiwa kubofya http://........................................ na kuingiza jina jumuishi na neno la siri kisha kubofya “ingia”;



# 7.0 MFUMO WA NDANI WA KUFANYIA KAZI MAOMBI YA USAJILI…

2. Kupitisha au kusitisha Maombi, baada ya kuingia Afisa atatakiwa kubofya “***Taarifa mbalimbali***”, “***hatua za maombi”***, “orodha ya maombi yaliyopokelewa” ***kisha bofya kitufe*** ndani ya “***Hatua***”



# 7.0 MFUMO WA NDANI WA KUFANYIA KAZI MAOMBI YA USAJILI…

3. Afisa atatakiwa kubofya “***Pitisha Maombi***” kwa yale yaliyokidhi vigezo au “***Sitisha Maombi”***, kwa yale yasiyokidhi vigezo;



# 7.0 MFUMO WA NDANI WA KUFANYIA KAZI MAOMBI YA USAJILI…

4. Endapo Afisa atasitisha maobi atatakiwa kuweka sababu za kusitisha na kisha atabofya ***“sitisha*”**



# 8.0 HITIMISHO

- Hatua za maboresho zinazochukuliwa sasa na Serikali zinalenga;

***Kuliandaa na kulikuza kundi hili la wafanyabiashara linalojishughulisha na kazi za kiuchumi ili siku za usoni, baada ya kukua kwa biashara zao, liingizwe kwenye wigo rasmi wa kodi kwa mujibu wa Sheria***

- Ni jukumu la kila mdau kushiriki kikamilifu kuwezesha ukuaji wa tabaka hili la wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo

# AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA

